

Kumtii Yesu Katika Nchi Nyingi

Soma Mathayo 28:19, 20. Wakristo leo wanatii kwa njia gani amri ya Yesu ya “kufanya wanafunzi kutoka kwa watu wa mataifa yote”? Jifunze kuhusu baadhi ya mataifa hayo kwenye ukurasa wa kwanza wa Tovuti ya jw.org/sw.

Mkiwa familia, angalieni kila picha iliyowekwa kwenye sehemu ya juu ya ukurasa huo. Jaribuni kukisia picha hiyo ni ya nchi gani. Kisha, bofya “FUNGUA” kwenye tovuti hiyo ili kujua ikiwa jibu lenu ni sahihi na kujua kuna Mashahidi wa Yehova wangapi wanaofundisha Biblia katika nchi hiyo. Halafu, angalieni ramani iliyopo hapa chini. Kwanza wekeni alama kuonyesha nchi mlizotazama ziko wapi kwenye ramani, kisha wekeni alama kuonyesha nchi mnamoishi.

► **SASA JARIBU KUFANYA HIVI:** Kwenye jw.org/sw, tafuta ofisi ya tawi ya Mashahidi wa Yehova (pia inaitwa Betheli) iliyo karibu na mahali mnapoishi. (Angalia chini ya KUTUHUSU > OFISI NA MATEMBEZI.) Chini ya “Mambo yenye kupendeza,” soma mambo yenye kutokeza kuhusu Betheli iliyo karibu nanyi.

